

Bibilia ya watoto  
Inawalettea

Miaka  
Arobaini



Kimeandikwa na: Edward Hughes

Kimeorodheshwa na: Janie Forest; Alastair  
Paterson

Imerekebishwa na: Lyn Doerksen


Kimetafsiriwa na: Bethel Children's Home,  
Kisumu, Kenya and Emmanuel Menya

Kimedhibitishwa na: Bible for Children  
[www.M1914.org](http://www.M1914.org)


©2021 Bible for Children, Inc.


License: Kuna ruhusa ya kuchapa hadithi hii,  
lakini bila ya kuuza.





Mungu alipowaokoa  
Waisraeli kutoka Misri,  
Musa akawaongoza watu  
katika kuabudu. Akatunga  
wimbo wa sifa. "Nitamwimbua  
BWANA kwa kuwa ametukuka  
sana." Musa akaimba matendo  
makuu yote Mungu  
aliyowafanyia  
Israeli.






Baada ya siku tatu  
jangwani watu wenye kiu  
wakapata maji. Lakini  
hawakuweza kunywa

maji machungu.






Badala ya kuomba,  
wakanung'unika.  
Mungu akawahurumia.  
Akayaponya maji


yakafaa kunywa.





Ikawa kama watu wananung'unikia kila kitu. Wakalia, "Tulikuwa na chakula Misri. Jangwani tutakufa kwa njaa."






Usiku huo Mungu akatuma ndege wanaoitwa kware. Watu wakawakamata kirahisi.



Asubuhi iliyofuata Mungu akatuma  
mana. Ilikuwa aina ya  
mkate wenye ladha  
kama biskuti za



asali. Kila  
asubuhi mana  
zilikuwa  
ardhini  
kwa ajili ya  
kuokotwa.






Kwa njia hii Mungu  
aliwalisha watu  
wake jangwani.



Walitakiwa kumtumaini Mungu kila siku kwa ajili ya chakula kipyaa. Lakini wengine wakakusanya mana ya ziada, ingawa Mungu alisema itaoza ikisazwa hata asubuhi.



Kama ilivyokuwa imenenwa, mana  
ya jana ikaingia mabuu -isipokuwa  
katika siku ya Sabato. Katika siku  
ile maalum ya saba  
watu



Mungu  
aliwalea  
Waisraeli  
jangwani.

Aliwapa  
chakula na maji -  
na kuwalinda  
dhidi ya  
maadui  
zao.




Waamaleki  
walipowashambulia,  
Israeli  
waliendelea  
kushinda...



...vita kadiri  
Musa alivyoinua  
fimbo kwa  
Mungu.





Mungu aliwaambia Waisraeli, "Mkitii sauti yangu mtakuwa watu wangu hasa."





Watu wakamwambia Musa, "Yote anayotuamuru Mungu tutayafanya." Wakakabili Mlima Sinai na kumngoja Musa alipoenda 3 kukutana na Mungu.







Musa  
alikuwa  
pamoja na  
Mungu kwa  
siku  
arobaini.





Mungu  
aliandika  
Amri Kumi  
kwenye  
vipande  
vya  
mawe.





Alimwambia  
jinsi  
anavyotaka  
watu  
Wake  
waishi.



1. "Usiwe  
na miungu  
mingine ila  
mimi."

2. "Usijifanyie  
wala  
kusujudia  
sanamu ya  
kuchonga."



3. "Usilitaje  
bure jina la  
BWANA."

4. "Ikumbuke  
siku ya  
Sabato,  
uitakase."

5. "Mheshimu  
baba yako  
na mama  
yako."



6. "Usiue."


7. "Usizini."

8. "Usiibe."

9. "Usishuhudie  
uongo."


10. "Usitamani."





Wakati Musa  
akiwa pamoja  
na Mungu juu  
ya Mlima Sinai  
Waisraeli  
wakafanya  
jambo baya  
sana.






Walimuagiza  
Haruni  
atengeneze  
ndama wa shaba -  
wakamuabudu  
badala ya Mungu.  
Mungu akakasirika  
sana. Na Musa  
pia akakasirika.







Musa alipoona  
ndama na watu  
wanacheza,  
akazitupa mbao  
chini akazivunja.  
Kwa hasira Musa  
akaiharibu sanamu  
ya dhahabu.  
Watu waovu  
walioiabudu  
wakauawa.



Mungu akatoa mbaao  
zingine mbili za  
mawe. Akamwambia  
Musa ajenge hema -  
hema kubwa lenye uzio  
kulizunguka - ambapo  
Mungu atakaa  
na watu  
Wake.




Wamuabudu Mungu mahali hapo. Nguzo ya wingu na moto ilionyesha kwamba Mungu alikuwa pamoja nao.



Walipokaribia Kanani, Musa akatuma wapelelezi kumi na wawili ili kuona nchi ambayo Mungu aliwaahidi watu Wake.



Wapelelezi wote walikubali kwamba  
ni nchi nzuri! Lakini wawili tu, YOSHUA  
na KALEBU, ndio waliamini wangeweza  
kushinda na kumiliki nchi hiyo kwa  
msaada wa  
Mungu.




Wapelelezi wengine kumi  
waliogopa miji imara  
na majitu  
yaliyopo  
katika  
nchi.

Waliomboleza  
wakisema, "Hatuwezi  
kuimiliki nchi hiyo."




Walisahau matendo  
makuu ya Mungu  
aliyotenda  
katika  
kuwaweka  
huru

kutoka  
Misri.




Watu wakawafuata wapelelezi kumi wasioamini. Wakalia na kujiandaa kurudi Misri. Hata wakajaribu kumuua Musa!






Mungu akaokoa uhai wa Musa. Kisha akawaambia watu, "Kwa miaka arobaini mtazunguka jangwani.



Kalebu tu na Yoshua, na watoto wenu wataishi ili kuingia nchi mliyoidharau."



Miaka Arobaini

Hadithi kutoka kwa Neno la Mungu, Bibilia,

inapatikana katika

Kutoka 15 hadi Hesabu 14

"Kufafanusha maneno yako kwatia nuru."

Zaburi 119:130



Mwisho



Hii hadithi ya bibilia inatueleza kumhusu  
Mungu wetu wa ajabu aliyetuumba na  
anayetaka tumjue.

Mungu anajua tumetenda mambo mabaya,  
anayoyaita dhambi. Adhabu ya dhambi ni  
mauti, lakini Mungu anakupenda sana hata  
akamtuma mwana wake wa pekee, Yesu, Ili  
afe msalabani na aadhibiwe kwa dhambi  
yako. Alafu Yesu akafufuka na kuenda  
nyumbani mbinguni! Ukimwamini Yesu na  
kumwomba msamaha kwa dhambi yako,  
Atakusamehe! Yesu atkuja na kuishi ndani  
yako, na utaishi naye milele.



Kama unaamini huu  
ni ukweli, Sema haya kwa Mungu:  
Mpendwa Yesu, ninaamini kuwa wewe ni  
Mungu, na ulifanyika mtu ili ufe kwa ajili  
ya dhambi zangu, ili niwe na maisha mapya,  
na siku moja nitaenda kuwa nawe millele.  
Nisaidie nikutii na niishi kwa ajili yako  
kama mtoto wako. Amina.

Soma bibilia na uzungumze na Mungu  
kila siku! Yohana 3:16

